Walimbwende wa Miss Grand Tanzania wafanya ziara ya mafunzo hifadhi ya Pande.

Design a site like this with WordPress.com

ENTERTAINMENT

Walimbwende wa Miss Grand Tanzania wafanya ziara ya mafunzo hifadhi ya Pande.

Date: August 14, 2025 Author: mtezamedia 0 Comments

Walimbwende wa Miss Grand Tanzania wafanya ziara ya mafunzo hifadhi ya Pande.

Na Beatus Maganja,
Dar es Salaam

Walimbwende 24 wanaoshiriki mashindano ya Miss Grand Tanzania 2025 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara, wamefanya ziara ya siku moja katika Hifadhi ya Pande iliyopo jijini Dar es Salaam tarehe 13 Agosti 2025 kwa lengo la kujifunza masuala ya uhifadhi na utalii wa ndani.

Ziara hiyo iliandaliwa kwa ushirikiano kati ya waandaaji wa Miss Grand Tanzania na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), ikiwa ni sehemu ya kuwawezesha walimbwende hao kujifunza masuala ya uhifadhi na utalii na kuwa mabalozi wa vivutio vya utalii wa ndani, hususan Hifadhi ya Pande.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Kaimu Kamanda wa Hifadhi ya Pande, PC Suleiman Keraryo, alisema hifadhi hiyo ni kivutio cha kipekee kilichopo katikati ya Jiji la Dar es Salaam, ambapo wageni hupata fursa ya kutalii na kujionea vivutio mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujifunza kuhusu historia ya hifadhi hiyo, bioanuwai na mchango wake katika uhifadhi wa mazingira na viumbe hai.

“Karibuni sana katika Hifadhi yetu ya Pande, hifadhi iliyo katikati ya Jiji la Dar es Salaam, ikiwa na wanyamapori wa aina mbalimbali na vivutio vingine lukuki. Hapa ni mahali sahihi kwenu kujifunza na kujionea rasilimali za nchi yenu,” alisema Keraryo.

Aidha, alibainisha kuwa mshindi wa Miss Grand Tanzania 2025 atateuliwa kuwa Balozi wa Hifadhi ya Pande, ambapo atashirikiana na TAWA katika juhudi za kuitangaza hifadhi hiyo pamoja na kuchochea utalii wa ndani, sambamba na kuunga mkono juhudi za Serikali katika sekta ya maliasili na utalii.

Mashindano ya fainali ya Miss Grand Tanzania yanatarajiwa kufanyika tarehe 16 Agosti 2025 katika Ukumbi wa Superdome, Masaki – Dar es Salaam.

Uongozi wa Hifadhi ya Pande pia umeeleza dhamira yake ya kuendeleza ushirikiano na waandaaji wa Miss Grand Tanzania kwa kuhakikisha kuwa walimbwende wanapata fursa ya kulala ndani ya hifadhi hiyo na kufanya mazoezi katika mazingira ya asili, ili kuongeza uelewa wao kuhusu uhifadhi wa mazingira.

Kwa upande wao, walimbwende wameeleza kufurahishwa na ziara hiyo, hususan kupata fursa ya kuona kwa ukaribu aina mbalimbali za wanyamapori waliopo hifadhini humo, sambamba na mapokezi mazuri kutoka kwa maofisa wa TAWA. Pia waliahidi kuwa mabalozi wa kuitangaza hifadhi hiyo kwa jamii.

Walimbwende wa Miss Grand Tanzania wafanya ziara ya mafunzo hifadhi ya Pande.

Ziara hiyo imeelezwa kuwa ni mwanzo wa ushirikiano endelevu kati ya TAWA na taasisi za kijamii, hususan zinazowalenga vijana, kwa lengo la kuongeza uelewa juu ya umuhimu wa kulinda mazingira na kuendeleza utalii wa ndani kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Share this:

X Facebook

Loading...

← PREVIOUS
Tanzania yajipanga kuwa Kitovu cha utengenezaji wa bidhaa na huduma migodini kusini mwa Jangwa la Sahara.

NEXT →
Utabiri wa hali ya hewa kwa saa 24 zijazo Agosti 14/2025.

LEAVE A COMMENT

Search

ARCHIVES

August 2025 (138)

July 2025 (222)

June 2025 (186)

May 2025 (185)

Walimbwende wa Miss Grand Tanzania wafanya ziara ya mafunzo hifadhi ya Pande.

- April 2025 (178)
- March 2025 (198)
- February 2025 (146)
- January 2025 (150)
- December 2024 (166)
- November 2024 (180)
- October 2024 (184)
- September 2024 (139)
- August 2024 (113)
- July 2024 (143)
- June 2024 (105)
- May 2024 (98)
- April 2024 (116)
- March 2024 (116)
- February 2024 (81)
- January 2024 (91)
- December 2023 (47)
- November 2023 (87)
- October 2023 (83)
- September 2023 (107)
- August 2023 (120)
- July 2023 (142)

Walimbwende wa Miss Grand Tanzania wafanya ziara ya mafunzo hifadhi ya Pande.

- June 2023 (151)
- May 2023 (160)
- April 2023 (134)
- March 2023 (146)
- February 2023 (100)
- January 2023 (62)
- December 2022 (88)
- November 2022 (78)
- October 2022 (62)
- September 2022 (52)
- August 2022 (54)
- July 2022 (63)
- June 2022 (34)
- May 2022 (27)
- April 2022 (33)
- March 2022 (30)
- February 2022 (13)
- January 2022 (17)
- December 2021 (20)
- November 2021 (32)
- October 2021 (43)

Walimbwende wa Miss Grand Tanzania wafanya ziara ya mafunzo hifadhi ya Pande.

- September 2021 (23)
- August 2021 (26)
- July 2021 (24)
- June 2021 (12)
- May 2021 (20)
- April 2021 (16)
- March 2021 (17)
- February 2021 (20)
- January 2021 (22)
- December 2020 (31)
- November 2020 (32)
- October 2020 (53)
- September 2020 (22)
- August 2020 (15)
- July 2020 (30)
- June 2020 (21)
- May 2020 (19)
- April 2020 (16)
- March 2020 (52)
- February 2020 (55)
- January 2020 (32)
- December 2019 (45)

Walimbwende wa Miss Grand Tanzania wafanya ziara ya mafunzo hifadhi ya Pande.

- November 2019 (45)
- October 2019 (32)
- September 2019 (44)
- August 2019 (61)
- July 2019 (115)
- June 2019 (93)
- May 2019 (54)
- April 2019 (161)
- March 2019 (272)
- February 2019 (144)
- January 2019 (126)
- December 2018 (107)
- November 2018 (109)
- October 2018 (43)
- September 2018 (149)
- August 2018 (149)
- June 2018 (89)
- May 2018 (67)

CATEGORIES

- Biashara

RECENT POSTS

Tukitumia Nishati Safi ya kupikia tutaokoa hekta 400,000 za Misitu zinazoteketea

Walimbwende wa Miss Grand Tanzania wafanya ziara ya mafunzo hifadhi ya Pande.

- Breaking News
- Economy
- Education
- Entertainment
- Health
- kimataifa
- Makala
- Makala michezo
- Newspapers
- picha
- Politics
- Social
- Sports
- Uncategorized

kwa mwaka – Mjiolojia Nsajigwa.

August 16, 2025

Waandishi wa Habari wafundwa kuelekea uchaguzi Mkuu, Kibanda, Meena, Kwayu waweka “mtu kati”.

August 16, 2025

Ajali Mgodini Nyandolwa: Watano waokolewa kati ya 25 waliofukiwa na kifusi.

August 15, 2025

Elimu ya Nishati Safi ya kupikia yawafikia Wanawake Mkoani Mbeya.

August 15, 2025

Utabiri wa hali ya hewa kwa saa 24 zijazo Agosti 15/2025.

August 15, 2025

BLOG STATS

404,875 hits

August 2025

M	T	W	T	F	S	S
				1	2	3
4	5	6	7	8	9	10
11	12	13	14	15	16	17
18	19	20	21	22	23	24
25	26	27	28	29	30	31

« Jul

Walimbwende wa Miss Grand Tanzania wafanya ziara ya mafunzo hifadhi ya Pande.

FOLLOW BLOG VIA EMAIL

Enter your email address to follow this blog and receive notifications of new posts by email.

Email Address

Follow

Join 3,421 other subscribers

© 2025 MTEZA MEDIA

WEBSITE BUILT WITH WORDPRESS.COM.